TANGAZO LA SERIKALI NA . 151 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,

(SURA YA 355)

---

# AMRI

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

---

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MALINGUMU YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Malingumu ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la Kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Mafinga.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MLNG 1 yenye majira - nukta 753368MS, 9082423KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.27 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MLNG 2 yenye majira - nukta 753162MS, 9082590KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.064 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MLNG 3 yenye majira - nukta 753202MS, 9082640KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.18 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MLNG 4 yenye majira - nukta 753346MS, 9082533KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata bonde kwa umbali wa kilomita 5.52 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MLNG 10 yenye majira - nukta 753742MS, 9082524KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.048 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MLNG 11 yenye majira - nukta 753477MS, 9082449KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.25 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MLNG 1 hadi ulipoanzia''

Dodoma
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*